International Research Journal of Rongo University (IJORU)
2026, VOL. 4, NO. 2, 86 – 94
ISSN: 3005-7221

Received 02/06/2026
Revised 31/07/2026
Accepted 19/10/2026

SEMANTIKI YA MAJINA YA WALUO NCHINI KENYA: MTAZAMO WA MAWASILIANO YA KIUTAMADUNI

[1]Jael Akinyi Owala*, [1]Carren Nyandiba, [1]James Ontieri

*Corresponding author: jaelowala@gmail.com

https://orcid.org/0000-0002-5124-8052; https://orcid.org/0009-0008-3499-6180; https://orcid.org/0000-0003-3316-5533

[1]Chuo Kikuu cha Rongo, Sanduku la posta 103-40404, Rongo, Kenya

Ikisiri

Majina ya watu katika jamii za Kiafrika hubeba maana zinazohusiana na utamaduni, historia na mazingira ya kijamii. Miongoni mwa Waluo wa Kenya, majina si alama za utambulisho pekee, bali pia huakisi mitazamo ya jamii kuhusu maisha na matukio yanayohusiana na kuzaliwa kwa mtoto. Ingawa tafiti mbalimbali zimechunguza majina ya Kiafrika kwa mitazamo tofauti ya kiisimu, tafiti chache zimejikita katika kuchanganua maana za majina ya Waluo kwa mtazamo wa kisemantiki. Makala hii inalenga kuchunguza ruwaza za kisemantiki katika majina ya watu miongoni mwa Waluo nchini Kenya ili kubainisha maana zinazojitokeza katika majina hayo. Data ilikusanywa kutoka orodha za majina katika afisi za usajili wa watoto katika Kaunti ya Migori, mahojiano ya wazungumzaji wa Dholuo, pamoja na maandishi kuhusu majina ya Kiafrika. Data zilichanganuliwa kwa kutumia Nadharia ya Ujinaishaji ya Mill (1970). Matokeo yanaonyesha kuwa majina ya Waluo huakisi matukio ya kuzaliwa, hali za kijamii, imani za kitamaduni na matarajio ya wazazi. Maana zilizobainika ni pamoja na maana za kibusishi, dhamirifu, kijamii na dhanishi. Makala hii inahitimisha kuwa majina ya Waluo huonesha uhusiano kati ya lugha, utamaduni na mawasiliano, na pia huhifadhi utambulisho na urithi wa kiutamaduni.

Maneno Muhimu: *Majina ya watu, Semantiki, Utamaduni, Mawasiliano ya kiutamaduni, Waluo wa Kenya*.

Utangulizi

Majina ya watu ni sehemu muhimu ya maisha ya kila siku katika jamii yoyote. Hutumika kutambulisha watu, huku pia yakibeba maana na majukumu muhimu katika jamii. Aidha, majina hutumika kama nyenzo ya mawasiliano ya kiutamaduni kwa kuwa huwasilisha imani, maadili, historia na uzoefu wa jamii kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Majukumu haya yanaweza kufanana au kutofautiana kati ya jamii moja na nyingine. Resani (2016) anaeleza kuwa mara nyingi majina hubeba maana ya kitu au dhana inayokumbusha jamii matukio muhimu ya kijamii.

Kila jamii lugha ina namna mahususi ya kuunda majina ya watu. Namna hii ya uundaji huongozwa na mitazamo ya kijamii pamoja na kanuni za kiisimu. Katika jamii nyingi, kuna mifumo ya ujinaishaji inayohusisha nyakati, majira, mpangilio wa kuzaliwa, matukio muhimu au watu mashuhuri. Kupitia mifumo hii, majina huanza kubeba maana tofauti katika jamii na hivyo kuwa sehemu muhimu ya mawasiliano ya kiutamaduni.

Chacha na Malangwa (2017) wanaeleza kuwa suala la maana limekuwa likijadiliwa kwa muda mrefu bila kupata jibu lenye mashiko. Ogden na Richards (1985) wanafasili maana kama uhusiano kati ya kitu kinachoashiria na kile kinachorejelewa, ambapo neno linaweza kuchukua nafasi ya kitu hicho. Vilevile, Obuchi na Sangili (2016) wanaonesha kuwa maana ni dhana changamani ambayo huweza kueleweka kwa namna tofauti kulingana na muktadha, na wakati mwingine jina moja linaweza kuwa na maana tofauti katika jamii tofauti. Hali hii inaonesha kuwa maana za majina haziishii katika utambulisho wa watu pekee, bali pia huchangia katika mawasiliano yanayoakisi utamaduni wa jamii husika.

Tafiti nyingi zimefanywa kuhusu ujinaishaji na zinaonesha kuwa majina huakisi maisha ya familia, mazingira yao na matarajio ya wazazi kwa watoto wao (Mensah, 2022; Essein, 1986; Lapidos, 2010; Mokala,

Received 02/06/2026
Revised 31/07/2026
Accepted 19/10/2026

2020; Mboya, 1997). Mandah na Joshua (2025) wanaeleza kuwa majina yanaweza kuwa na maana ya kidhana, ya kimaelezo au ya kileksika, lakini huwa na umuhimu zaidi pale yanapopata maana ya kiashiria au ya matumizi ya moja kwa moja katika jamii. Pia, jina la mtu linaweza kubeba maana ya kumbukumbu au likawa jina la kifamilia linalotolewa ili kumuenzi na kuhifadhi kumbukumbu ya mwanafamilia aliyekwisha kufariki. Hali hii inaonesha kuwa maana za majina ni sehemu ya mawasiliano ya kiutamaduni yanayobeba historia, kumbukumbu na utambulisho wa jamii.

Kwa upande wa Waluo wa Kenya, majina huundwa kwa kufuata kanuni fulani za lugha na utamaduni. Hata hivyo, jamii hii imekuwa ikipitia mabadiliko ya kijamii, kiutamaduni na kiteknolojia yanayoathiri matumizi na uelewa wa majina. Mabadiliko haya yanaweza kuathiri namna maana za majina zinavyowasilishwa na kufasiriwa katika jamii. Katika muktadha huu, makala hii inachunguza ruwaza za kisemantiki katika majina ya watu miongoni mwa Waluo wa Kenya, kwa kuzingatia maana zinazojitokeza katika majina hayo na uhusiano wake na mawasiliano ya kiutamaduni.

Msingi wa Nadharia

Uchanganuzi wa majina katika makala hii uliongozwa na Nadharia ya Ujinaishaji ya Mill (1970). Kwa mujibu wa Mill, jina la pekee ni alama inayomtambulisha mtu na hurejelea kinachopatikana katika ulimwengu halisi, badala ya kubeba maana ya kimaelezo. Mtazamo huu uliwezesha kuchunguza jinsi majina ya Waluo yanavyorejelea watu, matukio na mazingira ya kijamii, pamoja na kubainisha maana zinazojitokeza katika matumizi yake. Kwa msingi huo, nadharia hii ilitumika kufafanua uhusiano kati ya majina, maana na muktadha wa kijamii katika mawasiliano ya kiutamaduni miongoni mwa Waluo nchini Kenya.

Mbinu za Utafiti

Makala hii ilitumia muundo elezi kwa kuwa ililenga kueleza na kuchanganua ruwaza za ujinaishaji miongoni mwa Waluo kama zinavyojitokeza katika matumizi ya kila siku. Muundo huu ulimwezesha mtafiti kupata maelezo ya kina kuhusu namna majina yanavyobeba maana katika jamii. Kwa mujibu wa Kombo na Tromp (2006), utafiti elezi husaidia kueleza na kufafanua hali au matukio kama yanavyojitokeza katika mazingira halisi. Hivyo, muundo huu ulifaa katika kuchunguza ruwaza za ujinaishaji na maana zinazohusishwa na majina ya Waluo.

Data ya makala hii ilikusanywa katika Kaunti ya Migori nchini Kenya, hususan katika maeneo ya Suna Magharibi na Suna Mashariki. Maeneo haya yalichaguliwa kutokana na mwingiliano wa kijamii na kiutamaduni unaojitokeza katika matumizi ya majina. Aidha, matumizi ya Dholuo katika maeneo hayo yalitoa mazingira mwafaka ya kuchunguza ruwaza za ujinaishaji miongoni mwa Waluo. Makala hii ilijikita katika taaluma ya Onomastiki kwa kuangazia uhusiano kati ya majina, maana zake na mazingira ya kijamii yanayoathiri uteuzi wa majina.

Sampuli ya majina 20 iliteuliwa kwa kutumia usampulishaji kimaksudi. Majina hayo yalichaguliwa kwa kuwa yaliwakilisha ruwaza za ujinaishaji katika jamii ya Waluo na kuwezesha uchanganuzi wa maana zinazojitokeza katika majina hayo. Aidha, wazee wanne, wawili wa kiume na wawili wa kike, waliteuliwa kimaksudi kutokana na maarifa yao ya kiutamaduni, hususan kuhusu asili na maana za majina ya Waluo.

Data ilikusanywa kutoka orodha za majina katika afisi za usajili wa watoto, kutoka kwa wazungumzaji wa Dholuo pamoja na maandishi ya kitaaluma yanayohusu majina ya Kiafrika. Mbinu zilizotumika katika ukusanyaji wa data ni mahojiano na majadiliano ya vikundi yaliyoongozwa na maswali ya wazi. Mbinu hizi zilitumika kupata maelezo kuhusu maana za majina na sababu za uteuzi wake. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa kutumia mbinu ya kimaelezo kwa kuzingatia ruwaza na maana zilizojitokeza katika majina yaliyoteuliwa. Uchanganuzi ulihusisha maana za kihusishi, maana dhanishi, maana dhamirifu na maana za kijamii kwa kuzingatia muktadha wa matumizi ya majina hayo.

Matokeo ya Utafiti

Sehemu hii inawasilisha matokeo ya utafiti kwa kuchanganua majina yaliyoteuliwa kwa kuzingatia maana dhanishi, kihusishi, dhamirifu na kijamii. Uchambuzi huu unaonesha jinsi majina ya Waluo yanavyobeba maana zinazohusiana na maisha ya jamii husika. Aidha, matokeo yanaonesha kuwa majina hayo huakisi uhusiano uliopo kati ya lugha, utamaduni na mawasiliano ya kiutamaduni. Kupitia majina hayo, jamii huweza kuhifadhi na kuendeleza maarifa ya kiutamaduni, historia, imani

International Research Journal of Rongo University (IJORU)
2026, VOL. 4, NO. 2, 86 – 94
ISSN: 3005-7221
Received 02/06/2026
Revised 31/07/2026
Accepted 19/10/2026

pamoja na uzoefu wa maisha kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Majina Yaliyofungamana na Mazingira Maalum

Makala hii imeonyesha kuwa baadhi ya majina ya Waluo hupewa watoto kulingana na mazingira au hali iliyokuwepo wakati wa kuzaliwa kwao. Mazingira hayo yanaweza kuwa ya wakati, hali ya hewa, shughuli zilizokuwa zikiendelea au matukio yaliyotokea katika jamii katika kipindi hicho. Matokeo yanaonesha kuwa majina hayo hutumika kuhifadhi kumbukumbu za matukio na uzoefu wa maisha ya jamii. Kwa njia hii, majina huwa na maana pana inayozidi utambulisho wa kawaida, kwani huonesha uhusiano uliopo kati ya lugha, utamaduni na maisha ya kila siku ya jamii ya Waluo. Kwa mtazamo huu, mazingira ya kuzaliwa huwa sehemu ya ujumbe unaowasilishwa kupitia jina, hivyo kulifanya jina kuwa nyenzo ya mawasiliano ya kiutamaduni. Miongoni mwa majina yaliyobainika katika kundi hili ni Awiti/Owiti, Adero/Odero, Agola/Ogola na Agot/Ogot.

Awiti/ Owiti

Awiti ni jina linalopewa mtoto wa kike huku Owiti likipewa mtoto wa kiume. Majina haya hupewa watoto wanaozaliwa baada ya watoto waliowatangulia kufariki tumboni mwa mama au muda mfupi baada ya kuzaliwa. Katika lugha ya Dholuo, *wito* humaanisha kutupa, jambo linaloeleza msingi wa utoaji wa majina haya. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa katika jamii ya Waluo, mtoto anayezaliwa katika hali kama hii huchukuliwa kuwa amekuja baada ya kipindi cha huzuni na hofu kubwa katika familia. Kutokana na imani za jamii, mtoto huyo alikuwa akitwaliwa na mkunga na kutupwa nje ya boma kama ishara ya kufukuza pepo au mkosi uliodhaniwa kusababisha vifo vya watoto waliotangulia. Baadaye, mmoja wa wanajamii angemwokota mtoto huyo na kumrudisha nyumbani kama ishara ya kumpokea tena katika familia na jamii. Kwa maana dhanishi, Awiti/Owiti humaanisha mtoto ‘aliyetupwa’. Kwa maana kihusishi, jina hili linaashiria huzuni na hofu iliyotokana na vifo vya watoto waliotangulia, lakini pia linaibua matumaini ya mtoto huyo kuendelea kuishi. Kwa maana dhamirifu, wazazi walitumia jina hili kuonyesha tamanio lao la kumlinda mtoto dhidi ya mikosi iliyokuwa ikiandama familia. Kwa upande wa maana ya kijamii, jina hili linaonyesha imani, mila na mtazamo wa jamii ya Waluo kuhusu maisha, vifo na nguvu za kiroho.

Matokeo ya uchambuzi wa jina Awiti/Owiti yanaonesha kuwa majina katika jamii ya Waluo hayakuwa ya utambulisho pekee, bali yalibeba ujumbe kuhusu mazingira na maisha ya jamii husika. Hoja hii inaafikiana na mawazo ya Babane (2017), anayeeleza kuwa majina katika jamii za Kiafrika huashiria mambo yaliyo zaidi ya maana ya moja kwa moja. Mtazamo huu unaungwa mkono na Msanjila na wenzake (2010), wanaoeleza kuwa majina hupata maana kupitia lugha na utamaduni wa jamii husika. Kwa mujibu wa Nadharia ya Ujinaishaji, jina Awiti/Owiti linarejelea mazingira mahsusi ya kuzaliwa kwa mtoto na hivyo kudhihirisha jinsi majina yanavyobeba maana zinazotokana na tajriba za jamii. Hali hii inaonesha kuwa majina ni nyenzo muhimu ya mawasiliano ya kiutamaduni kwa kuwa huhifadhi na kuwasilisha imani na uzoefu wa jamii ya Waluo.

Adero/Odero

Adero ni jina linalopewa mtoto wa kike huku Odero likipewa mtoto wa kiume aliyezaliwa wakati ghala lilikuwa limejaa mazao baada ya mavuno. Katika lugha ya Dholuo, *dero* humaanisha ghala. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa katika jamii ya Waluo, mazingira yaliyokuwepo wakati wa kuzaliwa kwa mtoto yalikuwa na nafasi kubwa katika kumtaja. Mtoto alipozaliwa wakati familia ilikuwa ikihifadhi mazao ghalani, hali hiyo ilichukuliwa kama ishara ya baraka na ustawi katika familia. Ndiyo maana jina lake lilihusishwa moja kwa moja na hali hiyo ya wakati wa kuzaliwa. Hii inaonesha kuwa majina yalikuwa zaidi ya utambulisho; yalikuwa pia njia ya kuhifadhi kumbukumbu ya mazingira na hali ya maisha ya jamii. Kwa maana dhanishi, Adero/Odero humaanisha mtoto aliyezaliwa katika mazingira yanayohusishwa na ghala. Kwa maana kihusishi, jina hili huibua maana ya neema, furaha na mafanikio yaliyohusishwa na hali ya familia wakati wa kuzaliwa kwa mtoto. Kwa maana dhamirifu, wazazi walilitumia jina hili kuonesha shukrani na matumaini ya maisha mazuri kwa mtoto huyo. Kwa upande wa maana ya kijamii, jina hili linaonesha jinsi kilimo na mavuno yalivyokuwa sehemu muhimu ya maisha ya jamii ya Waluo na jinsi mazingira yalivyochangia katika utoaji wa majina.

International Research Journal of Rongo University (IJORU)
2026, VOL. 4, NO. 2, 86 – 94
ISSN: 3005-7221

Received 02/06/2026
Revised 31/07/2026
Accepted 19/10/2026

Agola/Ogola, Agot/Ogot

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa Agola ni jina linalopewa mtoto wa kike na Ogola mtoto wa kiume aliyezaliwa zizini mwa ng'ombe. Vivyo hivyo, Agot ni jina la mtoto wa kike na Ogot la mtoto wa kiume aliyezaliwa mlimani. Majina haya yanaonesha kuwa katika jamii ya Waluo, mahali alipozaliwa mtoto palikuwa msingi muhimu wa uteuzi wa jina. Kwa maana dhanishi, Agola/Ogola humaanisha mtoto aliyezaliwa zizini mwa ng'ombe, ilhali Agot/Ogot humaanisha mtoto aliyezaliwa mlimani. Kwa maana kihusishi, majina haya huashiria mazingira mahsusi ya kuzaliwa kwa mtoto na hivyo kubeba kumbukumbu ya mahali na hali iliyokuwepo wakati wa kuzaliwa. Kwa maana dhamirifu, wazazi na wanajamii walitumia majina hayo kuhifadhi taarifa kuhusu mahali pa kuzaliwa kwa mtoto na kuendeleza kumbukumbu hiyo katika jamii. Kwa upande wa maana ya kijamii, majina haya yanaonesha kuwa jamii ya Waluo ilitumia mazingira ya kuzaliwa kama msingi wa utoaji wa majina, hivyo kuyafanya majina kuwa njia ya kuhifadhi na kuwasilisha maarifa ya kiutamaduni kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Matokeo haya yanaafikiana na yale ya Essien (1986), kama alivyonukuliwa na Mensah (2000), anayeeleza kuwa miongoni mwa Waibibio, watoto hupewa majina kwa kuzingatia mazingira au mahali wanapozaliwa. Kwa mfano, *Orua* hutolewa kwa mtoto aliyezaliwa sokoni, *Akai* kwa mtoto aliyezaliwa msituni na *Inwan* kwa mtoto aliyezaliwa shambani. Matokeo haya yanaonesha kuwa matumizi ya mazingira ya kuzaliwa kama msingi wa utoaji wa majina si jambo linalopatikana katika jamii ya Waluo pekee, bali pia limebainika katika jamii nyingine za Kiafrika. Hata hivyo, majina na mazingira yanayohusishwa nayo hutofautiana kulingana na utamaduni na tajriba ya kila jamii. Kwa mujibu wa Nadharia ya Ujinaishaji, majina Agola/Ogola na Agot/Ogot yanarejelea moja kwa moja mazingira ya kuzaliwa kwa mtoto. Hivyo, majina hayo yanaonesha jinsi jamii ya Waluo ilivyotumia majina kuwasilisha taarifa kuhusu mazingira ya kuzaliwa na kuhifadhi kumbukumbu za kijamii, jambo linalodhihirisha uhusiano wa karibu kati ya lugha, utamaduni na mawasiliano ya kiutamaduni.

Majina Yanayotokana na Sifa, Tabia au Hali Fulani ya Watu

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa baadhi ya majina katika jamii ya Waluo yalitokana na sifa, tabia au hali fulani zilizowahusu watu katika jamii hiyo. Mara nyingi majina hayo yalipewa watoto au kutumiwa kumrejelea mtu kulingana na namna jamii ilivyomtazama mtu huyo au hali iliyojitokeza katika maisha ya kila siku. Kupitia majina hayo, jamii iliwasilisha mitazamo, maadili na uzoefu wake kuhusu wanajamii. Hivyo, majina hayo yalitumika kama nyenzo ya mawasiliano ya kiutamaduni kwa kueleza namna jamii ilivyowatazama watu na mazingira yao ya kijamii.

Silwal/ Lando/ Ondisore/ Jaber

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa baadhi ya majina katika jamii ya Waluo yalitokana na maumbile au sifa za mtoto wakati wa kuzaliwa. Majina hayo yalitumiwa kueleza namna jamii ilivyomtazama mtoto kwa kuzingatia mwonekano wake wa kimwili na uzuri wa uso. Silwal ni jina linalotumika kumrejelea mvulana mwenye ngozi nyeupe, huku Lando likitumika kwa msichana mwenye ngozi nyeupe. Vivyo hivyo, Ondisore ni jina linalotumika kumrejelea msichana mwenye sura nzuri, ilhali Jaber linatumika kwa msichana mrembo. Majina haya yalikuwa na matumizi maalumu na hayakutumiwa kwa jinsia zote. Lando, Ondisore na Jaber ni majina ya kike kwa sababu urembo wa kuvutia macho ni sifa inayohusishwa zaidi na jinsia ya kike katika mtazamo wa jamii hiyo. Mgawanyo huu wa majina unaonyesha namna jamii ya Waluo ilivyohusisha sifa za kimwili na jinsia katika matumizi ya majina.

Kwa maana kihusishi, majina haya humrejelea mtu kwa kuzingatia maumbile au sifa zake za kimwili. Kwa maana dhanishi, majina hayo huibua dhana ya uzuri, mvuto na upekee wa mtu katika jamii. Kwa maana dhamirifu, matumizi ya majina haya yanaweza kuonesha mtazamo au nia ya mtoaji wa jina katika kumtambulisha, kumsifia au kumtania mhusika kulingana na sifa aliyonayo. Kwa upande wa maana ya kijamii, majina haya yanaonesha kuwa jamii ya Waluo ilizingatia maumbile na sifa za watu katika matumizi ya majina na kuyatumia kama sehemu ya mawasiliano katika mazingira ya kijamii.

Matokeo haya yanaafikiana na yale ya Mokala (2020), aliyebaini kuwa katika jamii ya Basotho watoto walipewa

International Research Journal of Rongo University (IJORU)
2026, VOL. 4, NO. 2, 86 – 94
ISSN: 3005-7221
Received 02/06/2026
Revised 31/07/2026
Accepted 19/10/2026

majina kufuatia maumbile yao. Hivyo, matokeo haya yanaunga mkono hoja kwamba majina katika jamii za Kiafrika huakisi maumbile na sifa za mtoto. Kwa mujibu wa Nadharia ya Ujinaishaji, majina haya yanarejelea sifa mahsusi za wahusika na hivyo kudhihirisha namna jamii ya Waluo ilivyotumia majina kuwasilisha mitazamo yake kuhusu maumbile na uzuri. Hali hii inaonesha kuwa majina ni nyenzo muhimu ya mawasiliano ya kiutamaduni kwa kuwa huhifadhi na kuwasilisha maadili, mitazamo na namna jamii inavyowatazama wanajamii wake.

Majina Yanayotokana na Nyakati au Majira

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa baadhi ya majina katika jamii ya Waluo yalitokana na wakati au kipindi ambacho mtoto alizaliwa. Nyakati hizo zilihusisha asubuhi, mchana, jioni au usiku, kulingana na muda halisi wa kuzaliwa kwa mtoto. Utafiti umebaini kuwa jamii ya Waluo ilitumia majina kuhifadhi kumbukumbu ya wakati wa kuzaliwa kwa mtoto. Kwa njia hii, majina hayo hayakuwa ya utambulisho pekee, bali pia yalitumika kuwasilisha taarifa kuhusu mazingira ya kuzaliwa na kuhifadhi kumbukumbu za jamii kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Aidha, nyakati za kuzaliwa ziliweza kuambatana na hali na hisia mbalimbali za kijamii zilizohusishwa na tukio la kuzaliwa. Kwa mfano, kuzaliwa wakati wa usiku kulihusishwa na giza, baridi, hofu kuhusu usalama wa mama na mtoto, pamoja na changamoto za kupata msaada kwa urahisi wakati wa kujifungua. Hivyo, majina yaliyotokana na wakati wa kuzaliwa hayakurejelea muda pekee, bali pia yaliweza kubeba kumbukumbu ya hali na uzoefu wa kijamii ulioambatana na wakati huo. Baadhi ya majina yaliyobainika kutokana na wakati wa kuzaliwa ni Atieno au Otieno, ambayo huhusishwa na watoto waliozaliwa wakati wa usiku.

Atieno/ Otieno

Atieno ni jina linalopewa mtoto wa kike aliyezaliwa usiku, huku Otieno likipewa mtoto wa kiume aliyezaliwa usiku. Katika lugha ya Dholuo, *gotieno* humaanisha usiku. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa katika jamii ya Waluo, majina mengi yalitolewa kulingana na wakati mtoto alipozaliwa. Kwa maana kihusishi, Atieno/Otieno humaanisha mtoto aliyezaliwa usiku. Kwa maana dhanishi, jina hili hubeba kumbukumbu ya wakati wa kuzaliwa kwa mtoto pamoja na hali zilizohusishwa na kipindi hicho. Kwa maana dhamirifu, wazazi na wanajamii walitumia jina hili kuhifadhi taarifa kuhusu wakati wa kuzaliwa kwa mtoto. Kwa upande wa maana ya kijamii, jina hili linaonesha mitazamo na hisia zilizohusishwa na kuzaliwa wakati wa usiku. Katika mazingira ya jadi, usiku ulihusishwa na giza, baridi, hofu kuhusu usalama wa mama na mtoto, pamoja na changamoto za kupata msaada kwa urahisi wakati wa kujifungua. Hivyo, kuzaliwa usiku kulikuwa na uzito wa kijamii unaozidi kurejelea muda wa kuzaliwa pekee. Jina Atieno/Otieno, kwa hiyo, lilihifadhi si tu kumbukumbu ya wakati wa kuzaliwa, bali pia uzoefu na hali za kijamii zilizohusishwa na wakati huo.

Matokeo haya yanaafikiana na yale ya Essein (1986), anayeeleza kuwa majina yalitolewa kulingana na nyakati na majira yaliyohusiana na kuzaliwa kwa mtoto. Kwa mujibu wa Nadharia ya Ujinaishaji, majina haya yanarejelea wakati mahsusi wa kuzaliwa kwa mtoto na, wakati huo huo, yanaakisi hali na hisia zilizohusishwa na wakati huo katika jamii. Hivyo, jina Atieno/Otieno linaonesha jinsi jamii ya Waluo ilivyotumia majina kuhifadhi taarifa muhimu kuhusu wakati wa kuzaliwa pamoja na kumbukumbu ya mazingira na uzoefu wa kijamii uliouzunguka.

Majina Yanayotokana na Mfululizo wa Uzazi

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa katika jamii ya Waluo, baadhi ya majina ya watu yanahusishwa na mfululizo wa uzazi katika familia. Majina hayo huonesha nafasi ya mtoto katika mfuatano wa watoto wanaozaliwa na hivyo kuhifadhi taarifa kuhusu tukio la uzazi katika familia. Katika mfululizo wa uzazi, jamii ya Waluo hutumia majina kuonesha nafasi ya watoto katika tukio la kuzaliwa kwa mapacha.

Apiyo/ Opiyo na Adongo/ Odongo

Katika jamii ya Waluo, pacha wa kwanza hupewa jina Opiyo kwa mtoto wa kiume au Apiyo kwa mtoto wa kike, ilhali pacha wa pili hupewa jina Odongo kwa mtoto wa kiume au Adongo kwa mtoto wa kike. Majina haya huonesha mfuatano wa kuzaliwa kwa watoto wawili katika tukio la mapacha. Kwa hiyo, jina la mtoto linahusisha utambulisho wake na nafasi yake katika mfululizo wa uzazi. Kwa maana kihusishi, Opiyo/Apiyo humrejelea pacha aliyezaliwa kwanza, ilhali

International Research Journal of Rongo University (IJORU)
2026, VOL. 4, NO. 2, 86 – 94
ISSN: 3005-7221
Received 02/06/2026
Revised 31/07/2026
Accepted 19/10/2026

Odongo/Adongo humrejelea pacha aliyezaliwa baada yake. Kwa maana dhanishi, majina haya huibua dhana ya kufuatana kwa watoto katika tukio la uzazi. Kwa maana dhamirifu, wazazi na wanajamii hutumia majina haya kuwasilisha taarifa kuhusu mfuatano wa kuzaliwa kwa mapacha. Kwa upande wa maana ya kijamii, majina haya yanaonesha kuwa mfuatano wa uzazi ulikuwa sehemu ya taarifa muhimu katika kumtambua mtoto na kumweka katika nafasi yake ndani ya familia.

Matokeo haya yanaafikiana na Kayeli (2012), aliyebaini kuwa katika jamii ya Avogoli/Logoli wa Magharibi mwa Kenya, mapacha hupewa majina Mukhwana au Mulongo, huku mtoto anayezaliwa baada ya mapacha hao akiitwa Kisia. Ulinganisho huu unaonyesha kuwa majina yanayohusishwa na mfululizo wa uzazi yanapatikana pia katika jamii nyingine za Kenya, ingawa majina yanayotumiwa hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Kwa mujibu wa Nadharia ya Ujinaishaji, majina Apiyo/Opiyo na Adongo/Odongo yanarejelea nafasi ya watoto katika mfululizo wa uzazi wa mapacha. Majina haya yanaonesha namna jamii ya Waluo inavyotumia mfumo wa ujinaishaji kuhifadhi na kuwasilisha taarifa za kifamilia, na hivyo kudhihirisha uhusiano kati ya lugha, utamaduni na mfululizo wa uzazi.

Majina Yanayoakisi Imani za Kidini

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa baadhi ya majina katika jamii ya Waluo yanahusishwa na imani za kidini. Wazazi huweza kumpa mtoto jina linaloonesha namna wanavyotafsiri kuzaliwa kwake, hasa pale wanapoona mtoto huyo kama zawadi kutoka kwa Mungu, jibu la maombi au utimilifu wa ahadi waliyoweka. Kwa mfano, jina *Mich* au *Chiwo* humaanisha zawadi na huonesha kuwa mtoto anachukuliwa kuwa zawadi kutoka kwa Mungu. *Lamo* humaanisha dua au maombi na hutolewa hasa, kwa mtoto anayezaliwa baada ya wazazi kupitia changamoto ya kupata mtoto. Jina hilo kwa hiyo, linaonesha nafasi ya maombi katika ujio wa mtoto. Vilevile, *Singo* huhusishwa na ahadi au nadhiri iliyotolewa kwa Mungu kabla ya mtoto kuzaliwa. Jina *Yesu Nyalo*, linalomaanisha *Yesu anaweza*, huonyesha imani ya wazazi katika uwezo wa Yesu, hasa mtoto anapozaliwa baada ya kipindi kigumu cha ujauzito au kujifungua. Majina haya yanaonesha kuwa tukio la kuzaliwa kwa mtoto na imani ya wazazi vinaweza kuunganishwa katika jina lake.

Hali hii pia inaonekana katika majina kama *Angel Gabriel*, *Prosper*, *Goodwill* na *Jewel*. Jina *Angel Gabriel* linaonesha namna mtoto anavyothaminiwa na kuhusishwa na zawadi kutoka kwa Mungu. *Prosper* huonesha matarajio ya wazazi ya mafanikio katika maisha ya mtoto, wakati *Goodwill* huonesha matumaini mema waliyo nayo kuhusu maisha yake. Kwa upande mwingine, *Jewel*, lenye maana ya kito, humwonesha mtoto kama mtu wa thamani kubwa katika familia. Kwa hiyo, majina haya hayahusiani na imani ya kidini kwa namna moja tu; mengine huonesha shukrani kwa mtoto aliyepatikana, huku mengine yakibeba matarajio ya wazazi kuhusu maisha yake.

Kwa maana kihusishi, majina haya humrejelea mtoto kama zawadi, jibu la maombi, utimilifu wa ahadi au ishara ya uwezo wa Mungu. Kwa maana dhanishi, huibua imani, matumaini, shukrani na thamani anayopewa mtoto. Kwa maana dhamirifu, wazazi hutumia majina hayo kueleza imani yao na matarajio waliyonayo kuhusu mtoto. Kwa upande wa maana ya kijamii, majina haya yanaonesha nafasi ya imani za kidini katika maisha ya jamii ya Waluo. Jina linakuwa sehemu ya ujumbe unaohifadhi kumbukumbu ya tukio la kuzaliwa na mtazamo wa wazazi kuhusu mtoto.

Matokeo haya yanaafikiana na Lapidos (2010), anayeeleza kuhusu utamaduni wa ujinaishaji nchini Nigeria na kuonyesha kuwa majina yanaweza kuakisi mazingira ya kuzaliwa kwa mtoto pamoja na matarajio ya wazazi kuhusu maisha yake. Hoja hii inahusiana na majina yaliyobainika katika utafiti huu, hasa *Lamo*, *Singo* na *Yesu Nyalo*, kwa sababu majina hayo yanaunganisha mtoto na maombi, ahadi na imani ya wazazi. Ingawa jamii za Nigeria na Waluo zinatofautiana katika lugha na utamaduni, mifano hii inaonesha kuwa jina linaweza kutumika kuhifadhi ujumbe unaohusiana na tukio la kuzaliwa na matarajio ya wazazi.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Ujinaishaji, majina haya yanaonesha kuwa jina linaweza kubeba taarifa zaidi ya kumtambua mtu. Katika jamii ya Waluo, majina yanayoakisi imani za kidini huhifadhi imani, matumaini na uzoefu wa wazazi unaohusishwa na kuzaliwa kwa mtoto. Kwa mtazamo huu, jina linakuwa sehemu ya mawasiliano ya kiutamaduni kwa sababu hubeba ujumbe unaoweza kueleweka na wanajamii na kuendelezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

International Research Journal of Rongo University (IJORU)
2026, VOL. 4, NO. 2, 86 – 94
ISSN: 3005-7221
Received 02/06/2026
Revised 31/07/2026
Accepted 19/10/2026

Majina Yanayoakisi Athari za Elimu na Teknolojia

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa baadhi ya majina katika jamii ya Waluo yanaakisi athari za elimu na maendeleo ya teknolojia. Kupitia elimu, watu hupata maarifa mapya na fursa pana za kuwasiliana na watu kutoka jamii na tamaduni nyingine. Hali hii imepanua mitazamo ya wazazi kuhusu uchaguzi wa majina, kiasi kwamba hawategemei mila na desturi za jadi pekee, bali pia hupata msukumo kutoka katika elimu, vyombo vya habari, runinga, mitandao ya kijamii na majukwaa mengine ya kidijiti. Mabadiliko haya yamechangia kuibuka kwa majina yenye asili na maana tofauti na yale yaliyotumika kwa kawaida katika jamii ya Waluo.

Baadhi ya majina yaliyobainishwa katika utafiti huu ni *Becky, Delvine, Starich, Warren* na *Jalex*. Majina haya yanaonesha namna wazazi wanavyopata vyanzo vipya vya kuchagua majina kutokana na mazingira yao mapana ya kijamii na kiutamaduni. Aidha, baadhi ya wazazi walieleza kuwa waliwapa watoto wao majina kutokana na watu waliowavutia katika nyanja mbalimbali za maisha. Kwa mfano, jina *Fabregas* lilitokana na mwanasoka maarufu wa Kihispania ambaye mzazi alimpenda kutokana na mafanikio yake katika mchezo wa kandanda. Mzazi huyo alitamani kwamba mwanawe angeweza kufuata nyayo za mwanasoka huyo wa Kihispania hapo baadaye. Vilevile, jina *Serena Williams* lilichaguliwa baada ya mzazi kuvutiwa na mafanikio ya mchezaji huyo wa tenisi aliyekuwa akimfuatilia kupitia runinga. Mifano hii inaonyesha kuwa majina yanaweza kubeba matarajio ya wazazi pamoja na watu waliowavutia katika mazingira yao mapya ya kijamii na kiutamaduni.

Kwa maana kihusishi, baadhi ya majina haya hurejelea watu halisi waliowavutia wazazi katika nyanja mbalimbali za maisha. Kwa mfano, *Fabregas* na *Serena Williams* yanahusishwa na watu mashuhuri katika michezo. Kwa maana dhanishi, majina haya huonesha sifa ambazo wazazi wanatamani watoto wao wawe nazo, kama vile mafanikio, bidii na umahiri. Kwa maana dhamirifu, wazazi hutumia majina haya kueleza matarajio yao kwamba watoto wao wataweza kufuata nyayo za watu wanaowavutiwa nao. Kwa upande wa maana ya kijamii, majina haya yanaonesha mabadiliko katika vyanzo vya uteuzi wa majina katika jamii ya Waluo, ambapo elimu, teknolojia, vyombo vya habari na mawasiliano na tamaduni nyingine vinaendelea kuwa na nafasi katika ujinaishaji.

Matokeo haya yanaafikiana na Suzman (1994), anayeeleza kuwa mabadiliko ya ujinaishaji huenda sambamba na mabadiliko ya kijamii. Katika uchunguzi wake kuhusu ujinaishaji wa Kizulu, Suzman anaonesha kuwa mabadiliko katika jamii yanaweza kuonekana pia katika namna watu wanavyoteua na kutumia majina. Hoja hii inahusiana na matokeo ya utafiti huu kwa kuwa majina kama *Becky, Delvine, Starich, Warren* na *Jalex* yanaonesha mabadiliko katika vyanzo vya uteuzi wa majina miongoni mwa Waluo. Vilevile, Tualaulelei (2021) anaonesha kuwa majina ni sehemu muhimu ya utambulisho wa mtu na wa kijamii, hasa katika mazingira ya elimu. Kwa msingi huo, mazingira ya elimu yanaweza kuwapa watu fursa ya kupata maarifa mapya na kupanua mawasiliano yao na watu na tamaduni nyingine. Maarifa na mawasiliano hayo yanaweza kuonekana katika uchaguzi wa majina, kama inavyodhihirishwa na majina yaliyobainika katika utafiti huu. Aidha, matokeo yanaafikiana na Ahieieva (2024), anayesisitiza umuhimu wa etimolojia ya majina katika kuelewa ujinaishaji kama mchakato wa kijamii na kiutamaduni.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Ujinaishaji, majina haya yanaonesha kuwa vyanzo vya uteuzi wa majina katika jamii ya Waluo vinaendelea kupanuka kutokana na elimu, teknolojia na mawasiliano na tamaduni nyingine. Jina linaweza kuhifadhi kumbukumbu ya mtu aliyemvutia mzazi, sifa anazozithamini au matarajio aliyonayo kuhusu maisha ya mtoto. Hivyo, majina haya yanaendelea kuwa sehemu ya mawasiliano ya kiutamaduni kwa kuwa kupitia majina hayo wazazi huwasilisha matarajio, maadili na mitazamo yao kuhusu maisha ya watoto wao na jamii kwa ujumla.

Hitimisho

Matokeo ya makala hii yanaonesha kuwa majina ya Waluo yana maana zinazohusiana na mazingira ya kuzaliwa kwa mtoto, sifa au hali inayomhusu, mfululizo wa uzazi, imani za kidini na athari za elimu na teknolojia. Hivyo, jina si utambulisho wa mtu pekee, bali pia huhifadhi taarifa kuhusu tukio, uzoefu na mtazamo uliokuwepo wakati wa kulitoa. Uchambuzi umeonesha kuwa majina hayo hubeba maana kihusishi, dhamirifu, dhanishi na kijamii,

Received 02/06/2026
Revised 31/07/2026
Accepted 19/10/2026

jambo linaloonesha kuwa uteuzi wa jina huathiriwa na mazingira ambayo mtoto na familia yake wanaishi.

Kwa kuongozwa na Nadharia ya Ujinaishaji, utafiti huu umebaini kuwa uteuzi wa majina una uhusiano na mazingira ya kijamii, kiutamaduni na kihistoria ya Waluo. Pamoja na hilo, mabadiliko ya jamii yameleta mwelekeo mpya katika ujinaishaji wa kisasa. Elimu imewapa wazazi maarifa na fursa pana za kuwasiliana na watu na tamaduni nyingine, huku dini, vyombo vya habari na teknolojia zikitoa vyanzo vipya vya majina na maana zake. Matokeo yake ni kwamba baadhi ya maana zilizohusishwa na majina katika mazingira ya jadi zimeendelea kupanuka au kupata tafsiri mpya kulingana na mazingira ya sasa.

Kwa ujumla, majina ya Waluo yanaendelea kuwa sehemu muhimu ya mawasiliano ya kiutamaduni kwa sababu yanahifadhi taarifa kuhusu maisha ya familia na jamii. Hata hivyo, ujinaishaji haujawa mchakato usiobadilika. Mabadiliko ya kijamii na kiutamaduni yameendelea kuathiri namna wazazi wanavyoteua majina na maana wanazoyapa. Kwa hiyo, majina ya Waluo yanaonesha kwa wakati mmoja mwendelezo wa urithi wa kitamaduni na mabadiliko yanayoendelea katika jamii. Hali hii inaonesha kuwa ujinaishaji ni mchakato unaoendelea kubadilika kadiri mazingira ya jamii yanavyobadilika.

Mapendekezo

Kutokana na matokeo yaliyowasilishwa katika makala hii, inapendekezwa kuwa jamii iendelee kuelimishwa kuhusu maana na umuhimu wa majina ya asili. Kufanya hivyo kutasaidia kuhifadhi utambulisho, historia na urithi wa kiutamaduni wa Waluo, hasa katika kipindi hiki ambacho mabadiliko ya kijamii, elimu na teknolojia yanaendelea kuathiri namna majina yanavyochaguliwa. Wazazi pia wanashauriwa kuzingatia maana na asili ya majina wanayowachagulia watoto wao pamoja na uhusiano wake na utamaduni wa jamii. Hii haimaanishi kwamba majina mapya hayafai kutumiwa, bali wazazi wanapaswa kufahamu maana na chanzo cha jina kabla ya kulichagua.

Aidha, taasisi za elimu na watafiti wanapaswa kuendelea kuchunguza ujinaishaji katika jamii mbalimbali. Tafiti hizo zitasaidia kuelewa namna maana za majina zinavyobadilika kutokana na mazingira ya kijamii, kiutamaduni na kihistoria. Tafiti za aina hii zinaweza pia kutoa nafasi ya kulinganisha namna jamii mbalimbali za Kiafrika zinavyotumia majina na namna mabadiliko ya kijamii yanavyojitokeza katika ujinaishaji.

Mwisho, vyombo vya habari na majukwaa ya kidijiti vinashauriwa kutumia nafasi yake kuelimisha jamii kuhusu maana na asili ya majina. Badala ya kueneza zaidi mitindo ya majina ya kisasa, majukwaa haya yanaweza pia kutoa maudhui yanayowasaidia wazazi na vijana kuelewa historia na maana ya majina wanayotumia. Kwa njia hii, matumizi ya vyombo vya habari na teknolojia yanaweza kusaidia kuhifadhi maarifa ya kiutamaduni yanayohusiana na majina, huku yakikubali mabadiliko yanayoendelea katika ujinaishaji wa kisasa.

Marejeleo

Ahieiva-Karkashadze, V. O. (2024). The etymology of the English names and the peculiarities of their translation from English into Ukraine. https://doi.org/10.32782/2409-1154.2024.65.48

Babane, V. C. (2017). How language challenges affect the behavior of immigrant learners in the Foundation Phase at three schools in Gauteng, South Africa. *South African Journal of Childhood Education, 10*(1), 1–10. https://doi.org/10.4102/sajce.v10i1.331

Bryman, A. (2012). *Social research methods*. Oxford University Press.

Chacha, L. M., na Malangwa, P. S. (2019). *Semantiki*. Longhorn Publishers.

Kayeli, E. C. (2012). *The role and meaning of birth, naming, initiation, marriage and death rituals among the Logoli of Western Kenya in view of inculturating related sacraments in the Roman Catholic Church* [Doctoral dissertation, University of Nairobi].

Kombo, D. K., na Tromp, D. L. A. (2006). *Proposal and thesis writing: An introduction*. Pauline Publications Africa.

Mandah, S. S., na Joshua, S. F. (2025). The indicative mood in Ikwere: A pragmatic approach. *Journal of Natural Language and Linguistics, 3*(1), 132–137. https://doi.org/10.54536/jnll.v3i1.5016

Received 02/06/2026
Revised 31/07/2026
Accepted 19/10/2026

Mboya, P. (1997). *Luo kitgi gi timbegi: A handbook of Luo customs* (6th ed.). East African Educational Publishers.

Mensah, E., Alexander, J., na Ayeni, Q. (2022). The ethnopragmatic functions of Owe and Tiv personal names in Nigeria. *Language Sciences, 91*, Article 101474. https://doi.org/10.1016/j.langsci.2022.101474

Mill, J. S. (1970). What's in a name? In R. Smith (Ed.), *Readings in philosophy of language* (pp. 45–60). Oxford University Press.

Mokala, M. (2020). Basotho naming systems and practices: A sociolinguistic-onomastic approach. *International Journal of Linguistics, Literature and Translation, 3*(1). https://doi.org/10.3299/ijllt.

Msanjila, Y. P., Kihore, Y. M., na Massamba, D. P. B. (2010). *Isimu jamii sekondari na vyuo*. TUKI.

Obuchi, S. M., na Sangili, K. N. (2016). *Taaluma ya maana: Semantiki na pragmatiki*. Jomo Kenyatta Foundation.

Resani, M. (2016). Maana katika majina ya Wabena nchini Tanzania. *Mulika, 35*, 98–113.

Suzman, S. M. (1994). Names as pointers: Zulu personal naming practices. *Language in Society, 23*(2), 253–272. https://doi.org/10.1017/S0047404500017851

Tualaulelei, E. (2021). Agency and power in classroom names and naming practices. *Ethnography and Education, 16*(1), 18–30. https://doi.org/10.1080/17457823.2020.1716262